SHULE YA SKONDARI KISELU
P.O.BOX 8889
MOSHI

KUMB NA. KSS/AD/VOL.I/2017

JINA LA MWANAFUNZI________________________________

**YAH/; MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KISELU WILAYA YA HAI MKOA WA KILIMANJARO MWAKA**

1.0. Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/1/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/1/2021 ndani ya siku saba.

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1. Sare ya shule

(a) Sare ya shule hii ni kama ifuatavyo:-

**1. WAVULANA**

| AINA YA NGUO | IDADI | MAELEZO YA MSHONO (Kipande SWcha kitambaa kimeambatanishwa) |
|---|---|---|
| 1. SWETA | MOJA (1) | Mshono- lisiwe la kubana |
| 2. SHATI | MBILI (2) | Nyeupe mikono mifupui |
| 3. SURUALI | MBILI (2) | Mshono iwe na marinda mbili isiwe ya kubana |
| 4. TAI | MOJA (1) blue iliyo kolea (dark blue) | Tai ndefu bluu bahari |
| 5. T-SHIRT | MOJA (1) | Mshono maelekezo shuleni (isiwe imebana) |

- Viatu vya ngozi kamba pea mbili (viatu vya plastiki haviruhusiwi)
- Soksi byeupe pea mbili (2)

(b) Sare ya michezo ni bukta moja (1) rangi nyeusi, fulna moja (1), raba pea moja (1) rangi nyeusi.

**2. WASICHANA**

| AINA YA NGUO | IDADI | MAELEZO YA MSHONO (Kipande SWcha kitambaa kimeambatanishwa) |
|---|---|---|
| 1. SWETA | MOJA (1) | Mshono- lisiwe la kubana |
| 2. SHATI | MBILI (2) | Nyeupe mikono mifupi |
| 3. SKETI | MBILI (2) | Mshono iwe ndefu rangi ya bluu bahari |
| 4. TAI | MOJA (1) blue iliyo kolea (dark blue) | iwe ndefu rangi ya bluu bahari |
| 5. T-SHIRT | MOJA (1) | isiwe ya kubana |

- Viatu vya ngozi vya kamba pea mbili (viatu ya plastiki haviruhusiwi
- Soksi nyeupe pea tatu (3)

(c) Sare ya michezo ni bukta moja (1) rangi nyeupe fulana moja (1) raba pea moja (1) rangi nyeusi.

2.2. Vifaa vya darasani

- Kalamu 2, Madaftari makubwa (counter book 10)
- Masha la hisabati
- Dictationary ndogo English –Swahili

2.3. Vifaa vya chakula

- Kijiko kimoja (1)
- Sahani moja (1) rangi ya damu yam zee

2.4. Mchanganuo wa mchango wa chakula
Chakula: Wasiliana na kamati ya ckaula katika vikao shuleni

1. Lipa michango yote ya fedha kwenye akaunti namba 4013500128 NMB Hai Jina la akaunti ni Kiselu Sekondari.
2. Mwanao aje na hati ya malipo (bank pay slip) siku ya kufungua shule
3. FEDHA YA MCHANGO WOWOTE HAITAPOKELEWA SHULENI
4. Hakikisha umeandika jina sahihi la mwanafunzi katika stakabdhi ya malipo na kidato chake.
   Mfano: Dominiki Wilfred Urassa kidato cha kwanza 2021.
5. Unashauriwa kulipa malipo yote kukwepa usumbufu wa kwenda benki mara kwa mara.
6. Unashauriwa kulipa malipo yote benki mapema kuepuka foleni ndefu benki wakati wa kufungua shule.

**Sheria na kanuni za shule hii**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na 25 ya mwaka 1988 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwana 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo yaUfundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika bika shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule nilazima.
(c) Kuwahi katika kila shughuli na nyingine utakazopewa.
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo utakayopewa ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
(h) Kutunza mali ya umma

3.0. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule
(a) Wizi
(b) Uasherati na ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevio wa matumizi mabaya ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocane, mirungi, kubeli na kadhalika.
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(g) Kudharau bendera ya Taifa
(h) Kuoa au kuolewa
(i) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani ya na nje ya shule
(j) Kutoa mimba
(k) Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi
(m) Kuwa na simu ya mkononi

4.0. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi
(a) Fomu ya maelekezo ya awali ya mahitaji ya shule
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya wanafunzi na mkataba wa kutoshirikki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
(d) Fomu ya daktari (Medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu a shule mara utakapo ripoti shuleni.

5.0. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII.**

______________________________

**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
MOSHI

**KISELU SEKONDARI**
**FOMU K.K**

*Fomu hii iajzwe kwa usahihi na mzazi/mlezi katika sehemu yake na mwanafunzi katika sehemu yake na irudishwe shuleni siku ya udahili.*

Mimi ______________________ mzazi/mlezi wa mwanafunzi nimesoma/nimeelewa masharti yote yanayohusu mtoto wangu kuingia shule ya sekondari Kiselu.

Nitampatia mahitaji yote yanayotakiwa na nitashirikiana na walimu katika kumlea vizuri mtoto wangu ili apate kunufaika na elimu atakayo ipata shuleni.

sahihi ya mzazi/mlezi ______________________________
Anwani ya mzazi/mlezi S.L.P.____________ (Mji)________
Tarehe ____________________

Mimi ______________________________________________(mwanafunzi)natambua kuwa nina dhamana kubwa sana kupatiwa nafasi katika shule ya serikali. Naahidi kutii sheria za shule na nitajitahidi kuwa mwanafunzi mwema na mwene bidii na niodhamu katika kazi zote za mikono na kazi za darasani kwa muda wote nitakaoishi shuleni Kiselu sekondari.

Sitashiriki vitendo viovu, migomo au maasi ya aina yoyote. Naahidi uzalendo mbele, utovu wa nidhamu kwangu itakuwa mwiko.

sahihi ya mwanafunzi ______________________
Tarehe ____________________

**KISELU SEKONDARI**
**FOMU H.B**

## HABARI BINAFSI KUHUSU MWANAFUNZI

*Fomu hii ijazwe kwa usahihi na mzazi/ mlezi nairudishwe shuleni siku ya udahili.*

1. Jina la Mwanafunzi ______________________________ (Jina hilo ndilo litakalotumika siku zote bila kubadilika)
2. Tarehe ya kuzaliwa ______________________
3. Mahali alipozaliwa _____________ wilaya ya _________ mkoa ______________
4. Jina la baba mlezi ___________________________________
5. Mahali (baba) anapoishi sasa____________________________________
6. anuani ya baba mlezi_______________________________________
   SLP_____ MJI)______________________________________________
7. Jilna lamama/mlezi____________________________________________
8. Dini ya mama /mlezi_________________________________________
9. Dini ya baba/ mlezi____________________________________________
10. Dini ya nwanafunzi______________________________________
11. Kaziya baba/mlezi__________________________________________
12. Kazi ya mama /mlezi_______________________________________
13. Namba ya simu ya mzazi/mlezi____________________________________
14. Michezo anayoshiriki mwanafunzi ni__________,_________,______________
15. Mimi ________________________(mzazi/mlezi) ninathibitisha kuwa taarifa nilizo andika ni sahihi_______________(sahihi ya mzazi/mlezi) tarehe ________

**KISELU SEKONDARI**
**FOMU M.E.**

***Request for medical examination***

*This form is to be completed by A Medical Officer and should be submitted at school on the day of admission.*

Name of pupil ______________________________

Age ________________ sex ___________

The above named has been examined in respect of:-

A. STOOL ________________
B. URINE ________________
C. CHEST ________________
D. BLOOD ________________
E. EYES ________________
F. EARS ________________
G. PREGNANCY TEST __________
H. OTHERS ________________

I am satisfied that the above named pupil is fit/not fit to persue further studies in a secondary school.

________________

Signature

________________

Date

________________

Designation

________________

Station

________________

Stamp

________________